


**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KILUVYA S.L.P 30348 DAR ES SALAAM.**



JINA LA MWANAFUNZI.....

FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA-2023

Uongozi wa shule ya Sekondari **KILUVYA** unayo furaha kujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka **2023** katika shule ya Sekondari **KILUVYA** mwaka huu kama mwanafunzi wa kutwa. Hongera sana kwa kupata nafasi hii .

MAHALI SHULE ILIPO:

Shule ya Sekondari **KILUVYA**, Ipo mkoa wa Dar es salaam, wilaya ya Ubungo Kata ya KIBAMBA mtaa wa **KILUVYA** umbali kutoka barabara kuu kufika shuleni ni **MITA 400**.

MUDA WA KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe **09/01/2023** saa 1:00 asubuhi fika na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa.

MAHITAJI MUHIMU YAKUJA NAYO SHULENI

1. Sare ya Shule jozi mbili
2. Begi moja la kubeba madaftari
3. Mkebe wa vifaa vya hisabati
4. Madaftari 12 counter book (Quire 3 au 4) na madaftari 12 ya **Msomi** kwa ajili ya mazoezi
5. Kamusi (Dictionary) English to English.
6. Kalamu ya wino na risasi pamoja na rula
7. T-shirt, , raba nyeupe kwa ajili ya michezo
8. Sweta rangi ya kijivu.
9. Vitabu cha kiingereza (Mabala the farmer na Hawa the bus driver)
10. Flat file moja.

MAELEZO YA SARE YA SHULE:-

WAVULANA

- Mashati 2 meupe ya mikono mifupi yasiyo bana na yaliyoshonewa alama ya kidato husika bega la kushoto(tumia kitambaa cha suruali)
- Suruali za rangi ya kijivu iliyokolea (dark gray) yenye upana wa cm 18 chini na marinda mawili kila Upande (**MARUKUFU KUBANA SURUALI-MODO**)
- Soksi ya rangi nyeusi
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu (Buti au Travota haviruhusiwi)
- Nywele fupi sio kipara.
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Sare za michezo: T- shirt ya kijani jeshi yenye kola, raba nyeupe,
- Vest nyeupe za kiume 2, chupa ya maji 1 na kontena la chakula 1

WASICHANA

- Mashati meupe 2 ya mikono mifupi yasiyo bana na yaliyoshonewa alama ya kidato husika bega la kushoto(tumia kitambaa cha sketi)
- Hijabu ndefu ifike katikati ya mapaja na ishonewe alama ya kidato husika chini ya hijabu mkono wa kushoto
- Rangi ya Hijabu ni nyeupe.
- Sketi ya rangi ya kijivu iliyokolea (dark gray) rinda boksi kati na marinda mawili pembedi ndefu ifike kwenye kifundo cha mguu.
- Soksi rangi nyeupe
- Viatu vyeusi nya ngozi visivyo na kisigino kirefu.
- Nywele fupi sio kipara (**MARUFUKU KUSUKA**)
- Sare za michezo: T- shirt ya kijani jeshi yenyne kola, raba nyeupe, (kwa anayevaa hijabu atapewa maelekezo ya namna ya kuva T-shirt)
- Vest nyeupe za kike 2, ,chupa ya maji 1 na kontena la chakula 1

SHERIA ZA SHULE

A. Nidhamu kwa ujumla

1. Ni lazima mwanafunzi awahi shulenii asubuhi saa 1:00 na kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili.
2. Mwanafunzi yoyote haruhuswi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa darasa, wa zamuu au idara ya malezi.
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mzigo walimu au mtu ye yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yake popote pale akutanapo na watu wa aina hiyo.
4. Hairuhuswi kutumia **LUGHA CHAFU** miiongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
6. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote nya darasani na shughuli za michezo, na uzalishaji mali kwa mujibu wa ratiba.
7. Mwanafunzi ni lazima afanye mitihani ya masomo yote anayosoma shulenii hapa.
8. Mwanafunzi awapo shulenii haruhuswi kuwa na aina yoyote ya vitu vifuatavyo:- kucha ndefu, kupaka rangi, kuva cheni, hereni, nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kupaka dawa nywele n.k.
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani au nje ya shule awe amevaa nguo za heshima. Ni marufuku kuva nguo zinazobana, fupi na nyepesi.
10. Mwanafunzi haruhuswi kuja na nguo zaidi ya zile zilizotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule, ikiwemo sweta la rangi inayotakiwa.
11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwenye utawala juu ya uharibifu wa mali ya shule.
12. Ni marufuku mwanafunzi yoyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalumu au bila kupewa ruhusa:-
 - i. Shule za jirani na sehemu za biashara
 - ii. Nyumba zinazozunguka shule
 - iii. Vibanda nya biashara nje ya shule
13. Ni marufuku mwanafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
 - i. Baa na klubu za usiku
 - ii. Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanpokuwa na wazazi au walezi wao
14. Wawapo shulenii hawaruhuswi kumiliki vitu nya gharama kama simu za mikononi, laptop, redio, kamera, ipad, albamu za picha na CD.
15. Kila mwanafunzi anatakiwa kufanya bidii katika kila somo. Mwanafunzi ambaye atapata chini ya 50% mwisho wa mwaka atakariri darasa (atarudia)
16. Hakikisha ukimya wa hali juu unazingatiwa katika maeneo yote ya shule na ya kujifunzia hasa darasani, maktaba, maabara na kwenye koridos wakati wa vipindi.

17. Adhabu ya viboko inaruhusiwa kwa kosa linalostahili.
18. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea kiingereza nje na ndani ya darasa.
- 19. Mwanafunzi ye yote akikamatwa na kitu chochote kisichotakiwa **kitaharibiwa mbele yake**.**

B. MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIFANYA ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE

1. Kutochokuwa ripoti ya maendeleo yake ya nusu mwaka au mwaka.
2. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevyia
3. Aina zote za wizi na unyang'anyi
4. Aina zote za makosa ya kujamiiiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video , vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
5. Kupiga au kupigana.
6. Matumizi ya lugha chafu au matusi.
7. Makosa ya jinai
8. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine.
9. Kugoma au kuchochea mgomo (ghasia).
10. Kutohudhuria shuleni kwa muda wa siku 30 mfululizo bila taarifa.
11. Kudharau Bendera ya Taifa kwa kutohudhuria paredi.
12. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule, (Pia ikithibitika kutoa mimba)
13. Kudharau maagizo na maelekezo yatolewayo na viranja, walimu au Mkuu wa shule
14. Kuoa au kuolewa .
15. Kukuwadia wanafunzi mwenzie na mtumishi ye yote katika mambo ya mapenzi ndani na nje ya shule.
16. Kunyanya sa mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsi yake, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.
17. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
18. Kukataa adhabu kwa makusudi. Pia adhabu inaweza kutolewa na mwalimu au kiranya ye yote kwa mwanafunzi anayeonesha utovu wa nidhamu.
19. Kiharibu mali ya shule ikiwa ni pamoja na majengo, mali ya mtu au kundi la watu au **unifom**.
MARUFUKU KUSHONA MODO (**suruali modo itakatwa bila taarifa yoyote kwa mzazi**) Kosa likirudiwa itapelekea kufukuzwa shule.
- 20. Kukamatwa na simu, redio, kamera, ipad, albamu za picha na CD kwa mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.**

ZINGATIA: Kumbuka umekuja shule ikubadilishe na sio wewe kuibadilisha shule vile utakavyo.

C. WAJIBU WA MZAZI/ MLEZI

- Mzazi/ Mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shuleni anapoanza masomo
- Mzazi/ Mlezi anatakiwa kuandikisha majina ya watu wanne (4) na namba zao za simu watakao ruhusiwa kupata ripoti za mtoto akiwa shuleni na mawasiliyanu ya vikao, wito n.k
- Mzazi / Mlezi anatakiwa kuja kuchukua ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatopokelewa muhula unaofuata.
- Mzazi/Mlezi anatakiwa kufika shuleni kwa muda muafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule
- Mzazi/ Mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake badala ya kusubiri kuitwa ili kujenga mshikamano wa malezi.
- Mzazi / Mlezi amfahamu kwa jina na namba ya simu ya **mwalimu wa darasa la mtoto** wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.
- Mzazi anatakiwa kuhudhuria vikao vya shule na vile vya kamati ya wazazi

CHRISTINA P MWITA

MKUU WA SHULE

SIMU : 0785 900 146

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KILUVYA S.L.P 30348 DAR ES SALAAM.**



RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school education

1. Pupil full name age
2. Blood
3. Stool.....
4. T.B Test.....
5. Syphilis Test.....
6. Urine Examination
7. Eye Test
8. Chest Test
9. Ears Test
10. Spleen
11. Abdomen
12. Pregnancy (for girls only)


ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.

I certify that, the above pupil is suitable/ unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:

Name of medical officer Signature

Date Official stamp

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KILUVYA S.L.P 30348 DAR ES SALAAM.**



FOMU NAMBA 3: FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi
Uraia Dini
Tarehe ya kuzaliwa Mahali ulipozaliwa.....
Yatima/ Sio yatima / Mzazi mmoja (kata isiyohusika)
Shule aliyomalizia darasa la saba mwaka.....
Mkoa anaotoka Wilaya
Tarafa anayotoka Kata Mtaa
Jina la Mwenyekiti wa mtaa Simu
Michezo anayopenda

PICHA YA
RANGI YA
MWANAFUNZI

Nathibitisha kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pmoja na kuwa na bidii ya masomo.

Jina la Mwanafunzi Sahihi.....Tarehe.....

TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI

Jina la Mzazi/Mlezi 1.....
Uraia Simu.....
Jina la Mzazi/Mlezi 2.....
Uraia Simu.....
Anuani kamili ya unapoishi mjini DSM.....
Sehemu unayoishi Wilaya
Mtaakata

PICHA YA RANGI
MZAZI/MLEZI 1

MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/ MLEZI

Jina la mwajiri na idara.....
Anuani
Namba ya simu
Kazi ya Mzazi/ Mlezi
(Mfano: Karani, Meeja, Mwalimu, Mfanyabiashara n.k)

Mimi Mzazi/Mlezi wa ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Kinzudi katka kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shulen. Nitakuwa nafatila maendeleo ya mwanangu na kuchukua ripoti kila muhula kwa kuwa najua kufatilia maendeleo ya mwanangu ni wajibu wangu na nisivyofanya hivyo hatua za sheria zichukuliwe zidi yangu. Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

Jina la Mzazi/ MleziSahihi.....Tarehe.....